# MPENI BWANA

*Zaburi 95 (29ème D.TO/A)*

*M: Ami-Fidèle*







*1. Mwimbieni Bwana wimbo mpya*
*Mwimbieni Bwana, Nchi zote*
*Mwimbieni Bwana, lisifuni jina lake.*
*2. Siku kwa siku tangazeni wokovu wake*
*Elezeni utukufu wake katika mataifa*
*Maajabu yake katika makabila yote.*
*3. Mpeni Bwana, Enyi jamii za mataifa*
*Mpeni Bwana, sifa na ezi*
*Mpeni Bwana utukufu wa jina lake*
*4. Leteni matoleo, ingieni katika wanja zake*
*Mwangukieni Bwana mkivaa mavazi matakatifu*
*Tetemekeni mbele yake, ewe dunia yote.*
*5. Waambieni mataifa Bwana ni Mfalme*
*Amekaza ulimwengu usitikisike*
*Atawala mataifa kwa haki*
*6. Sifa zimwendee Baba, na Mwanae Yesu Kristu*
*Sifa kwa Roho Mtakatifu, Kiongozi wakanisa.*
*Kama ilivyo kuwa mwanzo, na sasa, na milele. Amina.*

Rodriguez NTUGULO-2018